**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANA**
**OFISI YA WAZIRI MKUU**
**TAWALA ZA MIKOA ZA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA MANISPAA KAHAMA**

**Kumb.Na KMC/L.40/8/154** **05 Februari, 2026**

# TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Mkurugenzi wa Manispaa ya Kahama anawatangazia Watanzania wenye sifa kuomba nafasi za kazi tatu (03) katika halmashauri hii baada ya kupata kibali kutoka Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa mchanganuo ufuatao:-

## 1.1 DEREVA DARAJA LA II - NAFASI 03

### 1.1.1 MAJUKUMU NA KAZI

i. Kukagua gari kabla na baada ya Safari ili kubaini hali ya usalama wa gari
ii. Kuwapeleka watumishi maeneo mbalimbali kwenye safari za kikazi
iii. Kufanya matengenezo madogo madogo ya gari
iv. Kufanya na kusambaza nyaraka mbalimbali pale inapohitajika
v. Kujaza na kutunza taarifa ya za safari zote katika daftari la safari
vi. Kufanya usafi wa gari na
vii. Kazi nyingine atazopangiwa na mwajiri

### 1.1.2 SIFA ZA MWOMBAJI

Kuajiriwa mwenye Elimu ya Kidato cha Nne na Leseni ya Daraja la C au E ya uendeshaji magari ambayo amefanyia kazi kwa muda usiopungua mwaka mmoja bila kusababisha ajali na pia awe na cheti kilichompatia sifa ya kupata madaraja husika. Vilevile, awe amehudhuria mafunzo ya msingi ya uendeshaji magari (Basic Driving Course) yanayotolewa na Chuo cha VETA au Chuo kingine kinachotambuliwa na Serikali.

### 1.1.3 NGAZI YA MSHAHARA

**TGS B**

**MASHARTI YA JUMLA**

i. Waombaji wote wawe ni Raia wa Tanzania na wenye umri wa kuanzia miaka18 na usiozidi miaka 45.

ii. Waombaji wawasilishe maelezo binafsi (Curriculum Vitae) yanayojitosheleza (Detailed CV) yenye Anuani na Namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya wadhamini watatu (Referees) wa kuaminika;

iii. Waombaji waambatanishe nakala za vyeti vya Kidato cha Nne au Sita, Taaluma na cheti cha kuzaliwa. Waombaji watakaowasilisha" Result Slip"," Statement of Results"," Provisional Results" au" Transcripts HAVITAKUBALIKA;

iv. Kwa Waombaji waliosoma nje ya Nchi, Elimu ya Kidato cha Nne au Sita wawasilishe uthibitisho kutoka Baraza la Mitihani la Tanzania (NECTA).

v. Kwa waombaji waliosoma Vyuo nje ya Nchi wawasilishe uthibitisho kutoka Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU);

vi. Barua ya maombi iliyosainiwa na Mwombaji inaweza kuandikwa kwa lugha ya Kiingereza au Kiswahili;

vii. Waombaji wenye mahitaji maalum (special needs/disability) wanatakiwa kuainisha kwenye maombi yao;

viii. Waombaji watakaowasilisha Taarifa za kughushi watachukuliwa hatua kwa mujibu wa Sheria za Nchi;

ix. Waombaji waliostaafishwa katika Utumishi wa Umma hawaruhusiwi kuomba. isipokuwa kama wana kibali kutoka kwa Katibu Mkuu Kiongozi;

x. Wasailiwa ambao majina yao yanatofautiana katika nyaraka zao wanapaswa kuwasilisha hati ya Kiapo cha kubadili jina (Deed Poll) iliyosajiliwa na Wizara ya Ardhi.

**xi.** Mwisho wa kuwasilisha maombi ni tarehe **18/02/2026**

xii. **MUHIMU:** Unakumbushwa kuambatanisha barua yako ya maombi ya kazi iliyosainiwa, pamoja na vyeti vya elimu. Barua zote za maombi ziandikwe kwa

**Mkurugenzi wa Manispaa,**
**Halmashauri ya Manispaa ya Kahama,**
**Barabara ya Boma,**
**S.L.P 472,**
**KAHAMA – Shinyanga**

.

Maombi yote yatumwe kwenye mfumo wa kielektroniki wa Ajira **(Recruitment Portal)** kupitia anuani ifuatayo; **https://portal.ajira.go.tz** (Anuani hii pia inapatikana kwenye tovuti ya Sekretarieti ya Ajira kwa kuingia sehemu iliyoandikwa **'Recruitment Portal').**

xiii. Maombi yatakayowasilishwa nje ya utaratibu ulioainishwa katika tangazo hili **HAYATAFIKIRIWA.**

**Limetolewa na:**

**MKURUGENZI WA MANISPAA**
**HALMASHAURI YA MANISPAA YA KAHAMA**